**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/135/NZ/2024/36**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000258**

**KATI YA**

**KITONGOJI CHA MAITSA ............................................................. MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) ........................... MLALAMIKIWA**

---

**TUZO YA MAKUBALIANO**

---

***(Imetolewa na Kamati ya Sheria na Utawala ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha 145 cha tarehe 12 mwezi Februari 2025)***

## 1.0 Maelezo ya Awali

Mnamo tarehe 21 mwezi Oktoba 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka Kitongoji cha Maitsa, kilichoko Wilaya ya Babati Mkoa wa Manyara, wakiwakilishwa na Bw. Gabriel Senga na Bw. Sifael G. Mbise, ("Walalamikaji") dhidi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ("Mlalamikiwa"). Walalamikaji wanalalamikia kucheleweshewa maunganisho ya huduma ya umeme toka mwaka 2018 ambapo mradi wa umeme kupitia Wakala wa Umeme Vijijini uliwafikia kijijini kwao.

Walalamikaji wanaeleza kuwa, wakati mradi wa kupeleka umeme vijijini umewafikia walihamasishwa kuweka miundombinu katika nyumba zao na kuwa tayari kupokea huduma ya umeme, lakini kumekuwa na sintofahamu nyingi za ucheleweshaji wa kuunganishiwa huduma. Walalamikaji wanaeleza zaidi kwamba wamefuatilia mara kadhaa ofisi za Mlalamikiwa Mkoa wa Manyara na hawakupata ufumbuzi wa malalamiko yao hadi sasa na hivyo walifikia uamuzi wa kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka (EWURA) kuiomba imuamuru Mlalamikiwa kuunganisha huduma ya umeme kwa wakazi zaidi ya ishirini (20) wanaokosa huduma wa kitongoji cha Matisa.

Baada ya kupokea malalamiko, tarehe 25 mwezi Novemba 2024, Mamlaka (EWURA), ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules GN No. 428/2020*)).

Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake tarehe 11 mwezi Disemba 2024, na kuieleza Mamlaka kwamba, kitongoji cha Matisa ni miongoni mwa vitongoji vilivyopo katika Kijiji cha Managhat, Kata ya Singe na ili kufikisha huduma ya umeme kumebakia umbali wa kama kilomita tatu (3) ambazo zinahitaji bajeti ili huduma iweze kuwafikia wakazi hao. Mlalamikiwa ameweka katika mpango wa bajeti wa mwaka ujao wa fedha 2025/2026 na sasa mpango huo uko katika ngazi ya Kanda unafanyiwa kazi.

Kikao cha usuluhishi kati ya Wadaawa kilifanyika tarehe 24 mwezi Januari 2025, katika ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Whiterose iliyoko mjini Babati Mkoa wa Manyara. Mwisho wa kikao cha usuluhishi, pande zote mbili zilikubaliana kwamba, Mlalamikiwa ataunganisha huduma ya umeme kwa wakazi wa Kitongoji cha Matisa kufikia tarehe 30 mwezi Oktoba 2025.

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 14 (4) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

## 2.0 Makubaliano

Pande zote mbili zimefikia muafaka kwamba Mlalamikiwa ataunganisha huduma ya umeme kwa wakazi wa Kitongoji cha Matisa kufikia tarehe 30 mwezi Oktoba 2025.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (5) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila pande itabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 12 mwezi Februari 2025.

..............................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**